**JARIDA BUNDADC-TOLEO NA 2.**

**Aprili-Mei 2021**

***JINSI MFUMO WA GoT-HOMIS KUBORESHA HUDUMA ZAAFYA NA KUINUA MAPATO KATIKA VITUO VYA AFYA BUNDA DC.***

***www.bundadc.go.tz***

**UTANGULIZI.**

Mfumo wa GoT-HOMIS ni mfumo wa kilectroniki ulianzishwa kwaajili ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kutole huduma za Afya.

Mfumo wa GoT-HOMIS umeweza kusaidi kurahisha shughuli za vituo vya kutolea huduma za afya pamoja kusimamia uzalishaji na uhifadhi wa taarifa na takwimu za wagonjwa,mapato na dawa .

Pia mfumo huu umeweza kusaidia urahisishaji upatikanaji wa Taarifa kwa haraka.

Aidha Mfumo wa GoT-HOMIS umeweza kuongeza ufanisi kwa watendaji na upatikanaji wa taarifa nakuongeza uwajibikaji.

Halmashauri ya Wilaya Bunda imeweza kufanikiwa kufunga Mfumo huu katika Vituo vitatu.

Hata hivyo Hamashauri imeendelea kutenga fedha katika bajeti kwaajili kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za Afya unafungwa mfumo huo.

Katika kutambua umuhimu wa upatikanaji wa taarifa za afya pamoja na Udhibiti wa mapato katika Hospitali,Vituo vya Afya na Zahati Serikali ilianzisha Mfumo wa Government of Tanzania Health Operations informations System(GoT-HoMIS)

Ambapo ulianza kutumika mapema 2017 na kiasi kikubwa umewezesha vituo vya Afya,Hospitali,Zahanati kuwezesha kukusanya mapato yake kikamilifu kwa njia ya kielectroni na upatikanaji wa taarifa.

Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imeendelea kutekeleza agizo hilo la Serikali kwa kufunga mfumo huo katika Vituo vya Afya vitatu ambavyo Kisorya, Ikizu na Kasahunga.

Mkurugenzi Mtendaji Bwa Amos Kusaja amesema kuwa kuanzishwa kwa mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa GoT-HOMIS,ambao umesaidia katika kukusanya mapato katika vituo vya Afya.

‘Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mpaka sasa imefunga mfumo huo katika vituo vitatu ambapo mpaka sasa tumeona mabadiliko ya mapato ya awali na sasa baada ya kutumia mfumo huo’.anasema Bw. Kusaja


Mganga mfawidhi wa Kituo cha Afya Ikizu Bi Secilia likawa Amesema kuwa Kituo cha Afya Ikizu awali kilifunga mfumo huo katika vitengo viwili ambavyo ni mapokezi na dirisha la dawa kwa sasa mfumo umesambaa katika vitengo vinne zaidi ambavyo ni Ofisi ya Mganga Mfawidhi,OPD,Maabara na Wodi ya Wazazi.

‘’Mfumo huu unagharama nyingi sana katika kufunga ila tunashukuru tumeweza kufanikiwa kufunga katika maeneo yote katika kituo chetu’.amesema Bi Likawa

Dkt Likawa ameeleza mafanikio yaliyopatikana baada ya kuanza kutumia mfumo wa GoT-HOMIS, ni kuongezeka kwa mapato kwa wastani wa Tshs.3,596,229.60 kwa miezi mitano ya mwazo ya matumizi wa mfumo ikiwa ni tofauti na miezi mitano kabla ya kabla ya matumizi ya mfumo iliyokuwa na wastani wa Tshs.2,408,784 ambapo tofauti yake ni Tshs.1,187,445 baada ya matumizi ya mfumo.

Pia mfumo wa GoT-HOMIS umefanya kuongezeka kwa idadi ya wagonjwa wanaokuja kupata huduma katika kituo hicho .

“Kabla ya mfumo huu haujafunga,kituo kilikuwa inahudumia wagonjwa wapatao 10 hadi 20 kwa siku kwa upande wa ‘OPD’ lakini kwa sasa kituo kinahudumia wagonjwa 50 kwa siku”amesemaa Dkt likawa



***Bwa.Jeromine Leone Mhasibu kituo cha Afya Ikizu***

dirisha moja la huduma kwenda jingine kwaajili ya huduma za kitabibu.


Aidha Dkt Mussa amesema kuwa mfumo huu umesaidia kwa kiasi kikubwa ongezeko la mapato kutoka 1,016,000 hadi 1,055,000.

‘Kwasasa mfumo huu umeweza kuleta kila mchanganuo wa huduma ambayo imesaidia kuongezeka kwa mapato kwani awali ukusanyaji wa mapato uliuwa hafifu”.anasema Mussa

Pia Dkt Mussa ameeleza kuwa kutokana na ongezeo la mapato kituo imeweza kujihakikishia upatikanaji wa Dawa kwa asilimia mia.

“Tumefaniiwa udhibiti mianya ya upotevu wa dawa na hakuna mgonjwa anayefika kituoni akaosa dawa’.amesema Dkt Mussa

Kwa Upande wake Mganga Mfawidhi kituo cha Afya Kisorya Dkt Yassin Mussa amesema mfumo wa GoT-HOMIS umesaidia kutambua idadi ya wagonjwa waliofika katika kituo cha afya pamoja na taarifa nyingine za matumizi ya dawa kutokana mfumo unatunza taarifa.



***Bwa. Selemani Mahindi wa kituo cha Afya Kisorya akiingiza taarifa za mgonjwa kwa upande wa Dawa.***

Dkt Mussa ameeleza zaidi kuwa kupita mfumo huu umeweza kusaidia wagonjwa kutopata shida kuzunguka na faili kutoka dirisha moja la huduma kwenda jingine kwaajili ya huduma za kitabibu.

huu umeweza kuleta kila mchanganuo wa huduma ambayo imesaidia kuongezeka kwa mapato kwani awali ukusanyaji wa mapato uliuwa hafifu”.anasema Mussa

Pia Dkt Mussa ameeleza kuwa kutokana na ongezeo la mapato kituo imeweza kujihakikishia upatikanaji wa Dawa kwa asilimia mia.

“Tumefaniiwa udhibiti mianya ya upotevu wa dawa na hakuna mgonjwa anayefika kituoni akaosa dawa’.amesema Dkt Mussa

Yoweli Matonde Mganga Mfawidhi kituo cha afya Kasahunga amesema uwepo wa mfumo wa GoT-HOMIS umeweza kuonesha tofauti na mifumo mengine kutokana kuwa wenyewe unauweza wa ufanya kazi hata pasipo na Mtandao na hivyo kuweza kutoa huduma wakati wowote.

‘utoaji huduma wakati wowote hata usipokuwa na mtandao imesaidia kutohairisha kwa utoaji wa huduma kama ilivyo wa mifumo mengine’.

Dkt Matonde Ameeleza zaidi kuwa mfumo umeweza uhifadhi taaarifa za wagonjwa zilizojitosheleza,ambapo mgonjwa taarifa zake za ugonjwa zinaweza uonekana kokote na kusaidiwa kutokana na historia ya sehemu ya mwisho aliopatiwa huduma.

“awali taaarifa za mgonjwa zilikuwa zinajirudia rudia’.amesema

Mbali na uboreshaji wa huduma mfumo pia umesaidia kuongeza mapato kutoka 902,000.00 hadi 2,486,000.00.



***Bi.Flontina Wanjiku (Kushoto) akiwa atika huduma ya mapokezi katika kituo cha Afya Kasahunga***

Mkazi wa Kisorya Bwa. Juma Kiboko ameishukuru serikali kwakuendele kuboresha huduma za afya ambapo kupiti mfumo wa GoT-HOMIS umeeweza kuondoa usumbufu kwa sisi wananchi hasa pindi unapofika hospital kuanza kutoa taarifa upya.

‘ila kwasasa tumeona mfumo unatunza taarifa ambapo ukifika kituo cha  huduma ni kueleza tatizo linalosumbua’.anasema Bwa.Kiboko

Ameeleza zaidi kuwa kupitia mfumo Serikali imeweza kuziba mianya ya upotevu wa mapato yake.

‘Awali mhudumu alikuwa anauwezo wa kujiamulia hii fedha niweke katika mfuko wa huduma au nisiweke ila sasa kila fedha inahifadhiwa’.anasema Bwa. Kiboko

Naye Mganga Mkuu wa Halmashauri Dkt Nuru Yunge ameishukuru Serikali kwa kuleta mfumo huo, kwa namna moja ama nyingine umeweza kutatua baadhi ya changamoto katika sehemu za kutolea huduma za afya katika Halmshauri ya Wilaya ya Bunda.

Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina Tarafa tatu ambazo ni Chamriho,Kenkombyo na Nansimo ina kata 17 na vijiji 78.

**WAHARIRI**

ALBERT CHUWA - MKUU WA KITENGO CHA TEHAMA

NURU ALLY - AFISA HABARI

EFRAIM-MWAKALOBO – AFISA TEHAMA